Boží svet – náš domov

Wiki ya maombi duniani | tarehe 3-4 mwezi wa sita 2023

Katka tafsiri nyingi za Biblia sentensi ya kwanza kabisa huanza na, “Hapo Mwanzo MUNGU ...” Kabla ya wakati, Mungu ni “Niko ambaye Niko”.

Ni Mungu ndiye aliweka utaratibu pasipo na utaratibu na kufanya uumbaji wa dunia. Ni yeye ndiye aliyempa mwanaume mamlaka ya kusimamia na kutawala uumbaji wake kwa msaada wa Mwanamke, kupitia ushirikiano unaoishi wa ndoa.

Mada yetu kwenye wiki ya maombi kwa mwaka 2023 inatufumbua macho kutambua kuwa tunaishi katika uumbaji wa Mungu: Ametufanyia mahali pazuri pakuishi.

Ni mahali pazuri ambapo tunatakiwa kuwajibika kwa kushirikiana ili kutoa faraja, kuhakikisha usalama na kuonyesha upendo kwa watoto wa zama hizi na kizazi kijacho.

Hebu tuelekeze maombi yetu kwa mwaka huu wa 2023 katika kuusifu uumbaji wa Mungu , kwa hatua za kujali uumbaji na kuhakikisha nasi tunaingilia kati kwa pamoja katika kutoa msaada kwa watoto walioathiriwa na tabia za uozo zilizojitokeza baada ya uumbaji. Uozo unaofanya kazi kutokana na mapungufu yetu wanadamu.

Kwa maana viumbe vyote pia vinatazamia kwa shauku nyingi kufunuliwa kwa wana wa Mungu. (Rumi 8: 19)

Ujumbe kutoka kwa Phil Green, Mtendaji mkuu wa Viva

“Baada ya kujiunga na viva kama mtendaji mkuu mwezi wa kumi na mbili mwaka 2022, Nina furaha kubwa kupongeza maandalizi ya maombi kwa mwaka huu wa 2023. Kwani inaangazia wito wangu wa kuwaona watoto wakituongoza katika kuomba na kumsifu Mungu”.

“Bwana Mungu wangu. Sikia kilio na maombi ambayo watumishi wako wanaomba mbele yako leo.” (1 Wafalme 8: 27)

Mwaka 2022, Zaidi ya watoto na watu wazima 800,000, kwenye nchi 25, walijumuika kushiriki maombi kwenye wiki ya maombi duniani. Nasubiri kwa hamu mwezi wa sita mwaka wa 2023 kuona watoto wengi wakija kwa pamoja kumsifu Mungu na kumsii atuepushe na changamoto mbalimbali zinazowakumba watoto: Yesu akajibu akasema , *“Yasiyowezekana kwa wanadamu yanawezekana kwa Mungu.” (Luka 18:27)*

MWANGA UKAJITENDA NA GIZA

SIKU 1

SOMA: Mwanzo 1: 1-5

SIFA ZA UUMBAJI: Mungu akaweka utaratibu**.** Umeme kwa ajili ya mwanga usiku.

KUJALI UUMBAJI: Vyanzo vinavyozalisha umeme mara kwa mara

KUJALI WATOTO KWA PAMOJA: Yesu kuangaza nuru ambapo giza la tabia mbaya ni tishio.

ZABURI 145: 'Ee Mungu wangu, Mfalme,nitakutukuza, Nitalihimidi jina lako milele na milele . Kila siku nitakuhimidi Nitalisifu jina lako milele na milele.' (Mstari wa 1-2)

KAZI: Tembelea https://youtu.be/EegzzyLlnZQ na kwa msaada wa Mrs Mukyala Moyler, make an Interplaylands Model world.

KUTENGANA KWA MAJI NA ANGA

SIKU 2

SOMA: MWANZO 1: 6-8

SIFA ZA UUMBAJI: Kwa mawingu yaletayo mvua

KUJALI UUMBAJI: Matumizi mazuri ya maji: mabwawa, umwagiliaji, pampu na mabomba.

KUWAJALI WATOTO KWA PAMOJA: Safisha maji ambayo hayajachafuliwa kwa ajili ya kunywa.

ZABURI 145: 'Bwana ndiye mkuu mwenye kusifiwa sana; wala ukuu wake hautambulikani . Kizazi kwa kizazi kitayasifu matendo yako, kitayatangaza matendo yako makuu. Nitayatafakari fahari ya utukufu wa adhama yako na matendo yako yote ya ajabu' (Mstari 3-5)

KAZI: Andaa orodha ya vivumishi vinavyoelezea uumbaji wa ajabu wa Mungu . Hifadhi na upime ujazo wa maji ya mvua.

ARDHI ILIYOUMBWA NA MITI, MATUNDA NA MIMEA

SIKU 3

SOMA: Mwanzo 1: 9-13

SIFA ZA UUMBAJI: Vilima na Mabonde kwa ajili ya makazi. Matunda na mboga za majani kwa ajili ya kula.

KUJALI UUMBAJI: Mavuno mazuri lakini kwa kuzingatia utunzaji wa udongo kwa siku zijazo. Punguza ukataji wa misitu.

KUJALI WATOTO KWA PAMOJA: Matunda na mboga za kutosha kwa watoto wanaokua.

ZABURI 145: 'Watu watayataja matendo yako ya kutisha, Nami-nitausimulia ukuu wako. Watalihubiri kumbukumbu la wema wako mkuu. Wataiimba haki yako kuu .Bwana ana fadhili, ni mwingi wa huruma, si mwepesi wa hasira ni mwingi wa rehema.' (Mstari wa 6-8)

KAZI: Panda mbegu – stawisha chakula .Tembea kwa asili –Kumbatia mti.

MCHANA, USIKU. JUA, MWEZI NA NYOTA.

SIKU 4

SOMA: Mwanzo 1: 14-19

SIFA ZA UUMBAJI: Kwa mwanga wa jua na majira .Kwa kasi ya mvutano unaoshikilia ulimwengu.

KUJALI UUMBAJI: Kupunguza ushawishi wa mwanadamu juu ya hali ya hewa.

KUWAJALI WATOTO KWA PAMOJA: Msaada kwa watoto na familia zilizo-

Athiriwa na majanga ya asili kama vile Moto,Ukame na Mafuriko.

PSALM 145: 'Bwana ni mwema kwa watu wote; Na rehema zake zi juu ya kazi zake zote. Ee Bwana kazi zako zote zitakushukuru, na wacha Mungu wote watakuhimidi. Wataunena utukufu wa ufalme wako na kuuhadithia uwezo wako,Ili kuwajulisha watu matendo yake makuu, na utukufu wa fahari ya ufalme wako .' (Mstari 9-12)

KAZI: Matembezi ya asili kutazama hali ya hewa, mwezi na nyota. Shughuli ndogo za kijamii ili kupunguza adhari za mafuriko.

SAMAKI NA NDEGE - KUZALIANA

SIKU 5

SOMA: Mwanzo 1: 20-23

SIFA ZA UUMBAJI: Uzuri wa samaki na Ndege. Jinsi zilivyowekwa kwenye mifumo sahihi . na baadaye zikafanyika zawadi ya Mungu kwa wanadamu kama chakula.

KUJALI UUMBAJI: Mamlaka kuzuia uvuvi uliopitiliza. Kutumia njia sahihi za uvuvi ili kufanya tuwe na samaki, nyama ya kuku na mayayi kwa siku zote.

KUJALI WATOTO KWA PAMOJA: Familia zote kuwa na Protein ya kutosha kwenye milo. Kuwalinda watoto dhidi ya maradhi yanayotokana na uzalishwaji wa vyakula.

PSALM 145: 'Ufalme wako ni ufalme wa zamani zote, Na mamlaka yako ni ya vizazi vyote. Bwana huwategemeza wote waangukao, huwainua wote walioinama chini. Macho ya watu wote yakuelekea wewe, Nawe uwapa chakula chao wakati wake.' (Mstari 13-15)

KAZI: Matembezi ya asili kuchunguza ndege wa angani. Fanya Litter pick – Punguza plastiki ndani ya bahari. Andaa mlo kamili pamoja.

VIUMBE VYOTE VYA ARDHINI. WANYAMA WA NYUMBANI NA-WANADAMU:

SIKU 6

SOMA: Mwanzo 1: 24-31

SIFA ZA UUMBAJI: Viumbe vya ardhini na muingiliano wao. Mume na Mke kwa ajili ya ndoa na watoto kwenye familia.

KUJALI UUMBAJI: Hekima katika kusawazisha mahitaji ya ongezeko la watu na wanyamapori. .

KUJALI WATOTO KWA PAMOJA: Ulinzi wa ndoa kwa kujawa na upendo, kujaliana na maelewano. Watoto ndani ya ndoa kutunzwa vizuri na kulelewa vyema.

ZABURI 145: Waufumbua mkono wako,Wakishibisha kila kilicho hai matakwa yake.Bwana ni mwenye haki katika njia zake zote na mwenye fadhili juu ya kazi zake zote . Bwana yu karibu na wote wamwitao, Wote wamwitao kwa uaminifu. Atawafanyia wamchao matakwa yao; naye atakisikia kilio chao na kuwaokoa.' (Mstari wa 16-19)

KAZI: A-Z ya wanyama (Cheza mchezo wa pamoja wa kupokezana kutaja majina ya wanyama wanaoanza na herufi tofauti tofauti za alfabeti).

SIKU YA MAPUMZIKO

SIKU 7

SOMA: Mwanzo 2: 1-3

SIFA ZA UUMBAJI: Mpango wa Mungu kutenga siku moja katika wiki kwa mapumziko na wakati wa kuzingatia ibada.

KUJALI UUMBAJI: Kujichunguza wenyewe: Tabia zetu za asili. Utaratibu mzuri na usawa wa kazi, Pumzika na Cheza.

KUJALI WATOTO KWA PAMOJA: Watoto katika miji wanaweza kufurahia siku nzuri za kawaida na maalum katika familia na upatikanaji wa kutosha wa maeneo ya kijamii.

ZABURI 145: 'Bwana huwahifadhi wote wampendao, Na wote wasio haki atawaangamiza. Kinywa changu kitazinena sifa za Bwana; Wote wenye mwili na walihimidi jina lake takatifu milele na milele.'
(Mstari 20-21)

TAFADHALI OMBA NASI:

1. MUNGU AUMBE DUNIA.



Asante Mungu kwa mwanga wa mchana na usiku. Asante Mungu kwa mwanga wako nyumbani kwangu.Asante Mungu kwa baraka zako za mvua. Tafadhali tuma mvua zako kwa wale ambao wanauhitaji mkubwa Ee Mungu muweza na muunbaji. Wewe ni mwenye nguvu. Asante kwa jinsi ulivyoumba dunia na namna ambavyo uliniumba pia.

2. MAKAZI YETU YANABOMOKA

Umeumba dunia kwa uzuri. Kila ulichokiumba umeumba kwa ukamilifu.
Tumekuwa wasumbufu katika dunia kwa sababu ya uzembe wetu na tamaa.
"BWANA Tusamehe!
Mungu wetu muumbaji,Ulitusii tuwe waangalivu juu ya bahari, lakini tayari tumeshajaza Takataka na uchafu wa kila aina .Tusamehe kwa sababu ya uzembe na ujinga wetu.

3. YESU JENGA UPYA.



Bwana Mungu, ulitupatia akili ya ajabu yenye uwezo wa kutatua matatizo na kupanga kwa upya. Nisaidie kubuni kwa upya sehemu ya kijani tena.
Mungu unayeishi, nisaidie kuwa mbunifu kama wewe.
Nisaidie kutengeneza makazi kwa ajili ya viumbe vyako au vitu mbalimbali.
Nisaidie kutambua njia nzuri ya kuhifadhi vitu ambavyo vimeshatumika tayari.

4. DUNIA YA MUNGU, MAKAZI YETU YAMEREJESHA



Mungu wetu muweza na Muumba wa ulimwengu, asante kwa kuja duniani na kunitafuta

Nilipokimbia mbali na wewe na kuacha maelekezo yako.
Asante Yesu, kwani wewe una nguvu juu ya viumbe vyote. Lakini umechagua kutufanya kuwa mawakili katika ulimwengu. Nisaidie niendelee kuwa wakili mwema

Prayers from the resource, 'Stewarding our world,' by Miriam Friday/Viva/CRANE in Uganda.

Artwork by: Vansh (13) India - day 1; Musinguzi (6), Uganda - day 2; Annalie (10) Germany - day 3; Jatin (16) India - day 4; Isabel (9) Cuba - day 5; Evie (12) UK - day 6.

The World Weekend of Prayer campaign is a global initiative held over the first weekend of June every year, uniting hundreds of thousands of adults and children globally. It is organised by Viva, a charity dedicated to changing more children's lives to fulfil their God-given potential in 42 community networks worldwide. Find out more at www.viva.org Registered charity no 1053389

viva
together for children